# (HEKIMA YA ALLAH (S.W) KWA NABII IBRAHIMU (A.S

<"xml encoding="UTF-8?>

BISMILAHI RAHMANI RAHIYMI

KWA JINA LA MWENYEEZI MUNGU MWINGI WA REHEMA MWENYE KUREHEMU

.(HEKIMA YA ALLAH (S.W) KWA NABII IBRAHIMU (A.S

Kisa cha Nabii Ibrahim (a.s) kinaonyesha Utukufu katika Miujiza ya Mwenyeezi Mungu, na Miujiza ni moja wapo miongoni mwa utukufu na hekima za Mwenyeezi Mungu katika nidhamu za kimaumbile, kwa sababu, kama tunavyojua kuwa vitu vyote ni vya Mwenyeezi Mungu basi athari ya vitu vyote hivyo pia ni ya Mwenyeezi Mungu, lakini baadhi ya wakati Mwenyeezi Mungu huleta muujiza ili kuthibitisha uhakika wa vitu hivyo, na baadhi ya wakati huleta athari .za kimaumbile katika kuthibitisha hayo

Mfano: Pale alipouamrisha moto uwe baridi kwa ajili ya Nabii Ibrahim (a.s), au kubadilika fimbo ya Nabii Mussa (a.s) na kuwa nyoka, na miujiza mengine mingi aliyoileta ili kuthibitisha utukufu .wake

قُلْنَا يَا نَارُ كُونِى بَرْداً وَسَلاَماً عَلـَي إِبْرَاهِيمَ[1]

!Sisi tukasema: Ewe moto! Kuwa baridi na salama kwa Ibrahim

قَالَ اَلْقِهَا يَا مُوسَي .  فَاَلْقَاهَا فَإِذَا هِيَ حَيَّةٌ تَسْعَي [2]

.Akasema: Itupe, ewe Musa! . Akaitupa. Mara ikawa nyoka anaye kwenda mbio

.HEKIMA ZA MWENYEEZI MUNGU KATIKA NIDHAMU ISIYO YA KIMAUMBILE

Milki na amri zake Mwenyeezi Mungu katika dunia nzima, ni dalili iliyo wazi kabisa inayoonesha hekima ya Mwenyeezi Mungu katika nidhamu isiyo ya kimaumbile. Kama tunavyosoma katika -:Qur-ani

مَا تَعْبُدُونَ مِن دُونِهِ إِلاَّ اَسْمَاء سَمَّيْتُمُوهَا اَنتُمْ وَآبَآؤُكُم مَّا اَنزَلَ اللّهُ بِهَا مِن سُلْطَانٍ إِنِ الْحُكْمُ إِلاَّ لِلّهِ اَمَرَ اَلاَّ تَعْبُدُواْ إِلاَّ إِيَّاهُ ذَٰلِكَ الدِّينُ الْقَيِّمُ وَلَـكِنَّ اَكْثَرَ النَّاسِ لاَ يَعْلَمُونَ[3]

Hamuabudu badala yake ila majina tu mliyo yapanga nyinyi na baba zenu. Mwenyezi Mungu

.hakuyateremshia hayo uthibitisho wowote

Hapana hukumu ila ya Mwenyezi Mungu tu. Yeye ameamrisha msimuabudu yeyote isipo kuwa .Yeye tu

.Hiyo ndiyo Dini Iliyo Nyooka. Lakini watu wengi hawajui

Anawabainishia baadhi ya Tawhiyd ya Mwenyeezi Mungu, mtu huchukua fursa ya kufundisha* .popote anapopatia wasaa. Usiitupe fursa ukiipata. Usije ukajuta

Kwa hiyo mmiliki wa haki wa vitu vyote duniani vya siri na vya dhahiri. Na Yeye ndiye anayejua mwanaadaamu anahitajia nini, basi Yeye ndiye m-bora katika kuweka kanuni zake na -:kuhukumu kutokana na hukumu hizo. Mwenyeezi Mungu anasema

اَفَحُكْمَ الْجَاهِلِيَّةِ يَبْغُونَ وَمَنْ اَحْسَنُ مِنَ اللّهِ حُكْماً لِّقَوْمٍ يُوقِنُونَ[4]

Je, wao wanataka hukumu za Kijahiliya? Na nani aliye mwema zaidi katika kuhukumu kuliko ?Mwenyezi Mungu kwa watu wenye yakini

Hapa wanahadidiwa wanaokataa hukumu alizotoa Mwenyeezi Mungu, wakakhitari mila ya * kienyeji (customary laws and decrees), na wako watu namna hii, basi wamo katika hatari .kubwa kabisa

Ni juu ya kila muislamu kuridhia aliyoyasema Mwenyeezi Mungu katika Qur-ani yake na aliyoyasema Mtume katika hadithi zake, akiyakataa haya basi kisha kusimama katika ukingo .wa moto wa jahannam tayari kutumbukia

Na kwa sababu hiyo basi Mwenyeezi Mungu Mtukufu anawataabiria wale watu ambao -:wanahukumu kile ambacho Mwenyeezi Mungu hajakiteremsha, kwa kusema

إِنَّا اَنزَلْنَا التَّوْرَاةَ فِيهَا هُدًى وَنُورٌ يَحْكُمُ بِهَا النَّبِيُّونَ الَّذِينَ اَسْلَمُواْ لِلَّذِينَ هَادُواْ وَالرَّبَّانِيُّونَ وَالاَحْبَارُ بِمَا اسْتُحْفِظُواْ مِن كِتَابِ اللّهِ وَكَانُواْ عَلَيْهِ شُهَدَاء فَلاَ تَخْشَوُاْ النَّاسَ وَاخْشَوْنِ وَلاَ تَشْتَرُواْ بِآيَاتِي ثَمَناً قَلِيلاً وَمَن لَّمْ يَحْكُم بِمَا اَنزَلَ اللّهُ فَأُوْلَـئِكَ هُمُ الْكَافِرُونَ[5]

Hakika Sisi tuliteremsha Taurati yenye uwongofu na nuru, ambayo kwayo Manabii walio nyenyekea kiislamu, na wachamngu, na wanazuoni, waliwahukumu Mayahudi; kwani .walikabidhiwa kukihifadhi Kitabu cha Mwenyezi Mungu

Nao wakawa ni mashahidi juu yake. Basi msiwaogope watu, bali niogopeni Mimi. Wala

msibadilishe Aya zangu kwa thamani chache. Na wasio hukumu kwa aliyo teremsha Mwenyezi .Mungu, basi hao ndio makafiri

Hapa inasifiwa Taurati kitabu cha Nabii Mussa kuwa kitabu hicho ijapokuwa aliteremshiwa* Nabii Mussa lakini Mitume wengi kabisa wa Kiyahudi waliokuja baada ya Nabii Mussa waliambiwa wakifuate hiki hiki, basi kikatumiwa na chungu ya Mitume na chungu ya .wanavyuoni na chungu ua wacha Mungu

Na juu ya hivi chungu ya Mayahudi walikipinga, na mwisho wakageuza geuza watakavyo. Na katika aya nyengine watu hao wametajwa kwa jina la dhalimu na fasiqi, pale Allah (s.w) -:aliposema

وَكَتَبْنَا عَلَيْهِمْ فِيهَا اَنَّ النَّفْسَ بِالنَّفْسِ وَالْعَيْنَ بِالْعَيْنِ وَالاَنفَ بِالاَنفِ وَالاُذُنَ بِالاُذُنِ وَالسِّنَّ بِالسِّنِّ وَالْجُرُوحَ قِصَاصٌ فَمَن تَصَدَّقَ بِهِ فَهُوَ كَفَّارَةٌ لَّهُ وَمَن لَّمْ يَحْكُم بِمَا انزَلَ اللّهُ فَاُوْلَـئِكَ هُمُ الظَّالِمُونَ[6]

Na humo tuliwaandikia ya kwamba roho kwa roho, na jicho kwa jicho, na pua kwa pua, na sikio kwa sikio, na jino kwa jino, na kwa majaraha kisasi. Lakini atakaye samehe basi itakuwa ni .kafara kwake

.Na wasio hukumu kwa yale aliyo yateremsha Mwenyezi Mungu, basi hao ndio madhaalimu

وَلْيَحْكُمْ اَهْلُ الإِنجِيلِ بِمَا اَنزَلَ اللّهُ فِيهِ وَمَن لَّمْ يَحْكُم بِمَا اَنزَلَ اللّهُ فَاُوْلَـئِكَ هُمُ الْفَاسِقُونَ[7]

Na wahukumu Watu wa Injili kwa yale aliyo teremsha Mwenyezi Mungu ndani yake. Na wasio .hukumu kwa yale aliyo yateremsha Mwenyezi Mungu basi hao ndio wapotofu

Hapa zinatajwa baadhi ya hukumu zilizokuwamo humo, na inatajwa Injili, kitabu* alichoteremshiwa Nabii Issa juu ya kuambiwa afuate na Taurati pia. Hii Injili ilikuwa ina .mawaidha zaidi kuliko hukumu

Na Taurati ina hukumu nyingi zaidi kuliko mawaidha, ilivyokuwa mwishowe Mayahudi wameharibika sana ndiyo hiyo Injili ikajazwa mawaidha hivyo ili zilainike kidogo nyoyo za .Mayahudi lakini wapi

Na huyu Nabii Issa alipelekwa kwa Mayahudi vile vile kama Nabii Mussa, si kwa Wazungu ila wengi kabisa walikataa kumfuata, akafuatwa na Wazungu kwa kulinganiwa na hao Mayahudi .waliomfuata

Hawa Wazungu wamefuata nyuma, baada ya kuondoka ulimwenguni nabii Issa (a.s) kwani dini .ya Mweenyeezi Mungu haina wenyewe makhsusi

Basi natija tunayoipata katika maelezo hayo ni kwamba Mwenyeezi Mungu ndiye mmiliki wa kila kitu duniani, na kwa wale watu ambao wanadai kuwa wao wamiliki Mwenyeezi Mungu -:anawambia

يُولِجُ اللَّيْلَ فِى النَّهَارِ وَيُولِجُ النَّهَارَ فِى اللَّيْلِ وَسَخَّرَ الشَّمْسَ وَالْقَمَرَ كُلٌّ يَجْرِى لِاَجَلٍ مُّسَمًّى ذٰلِكُمُ اللّٰهُ رَبُّكُمْ لَهُ الْمُلْكُ وَالَّذِينَ تَدْعُونَ مِن دُونِهِ مَا يَمْلِكُونَ مِن قِطْمِيرٍ[8]

Anauingiza usiku katika mchana, na anauingiza mchana katika usiku. Na amelifanya jua na .mwezi kutumikia. Kila kimoja wapo kinakwenda kwa muda maalumu

.Huyo ndiye Mwenyezi Mungu Mola wenu Mlezi

.Ufalme ni wake. Na hao mnao waomba badala yake hawamiliki hata ugozi wa kokwa ya tende

Surat Al-Anbiyaa aya ya 69 [1]

Surat Taha Aya ya 19-20 [2]

Surat Yussuf Aya ya 40 [3]

Surat Maidah Aya ya 50 [4]

Surat Al-Maidah Aya ya 44 [5]

Surat al-Maidah Aya ya 45 [6]

Surat al-Maidah Aya ya 47 [7]

Surat faatir Aya ya 13 [8]

MWISHO